NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

19 Machi 2025

Kwa Wabahá'í wa Ulimwengu

Marafiki wapendwa sana,

1. Asili ya jumuiya zinazoshamiri ambazo ulimwengu wa Kibahá'í unajitahidi kuzijenga ina athari kubwa kwa familia. Ni ndani ya familia ambamo mtu anazaliwa na kulelewa, na ni ndani ya familia ambamo watu huanza kujifunza jinsi ya kuishi pamoja na wengine. Kipengele cha familia ndiyo tofali la msingi la ujenzi wa jumuiya, na mbali zaidi, la utaratibu mzima wa kijamii. Kwa hiyo, jamii iliyoundwa ili kukidhi mahitaji ya zama za ukomavu wa mbari ya binadamu inahitaji vyote viwili; dhana komavu ya familia na uwezo wa kupanua umaizi unaotokana na dhana hiyo hadi kwenye uhusiano unaobumba sura ya taifa na dunia. “Familia ni taifa kwa mfano mdogo,” ‘Abdu’l-Bahá hueleza. “Hali zinazoikabili familia hulikabili taifa.” Kujifunza kuhusu mtindo mpya wa maisha ya familia, kwa hiyo, ni sehemu muhimu ya juhudi za kujifunza kuhusu uachiliwaji wa nguvu ya Imani ya ujengaji jumuiya.

2. Kihistoria, familia imechukua sura mbalimbali katika kuitikia mahitaji ya hatua mbalimbali za maendeleo ya kijamii ya binadamu. Kadiri jamii ilivyopiga hatua, mipango na maelekezo ambayo huenda yangekuwa ya manufaa katika nyakati zilizopita yangefikia ukomo wao na yasingefaa tena katika hatua ifuatayo ya maendeleo ya binadamu. Matarajio ya wazazi yaliyokuwa yenye kufaa kwa kipindi kimoja cha historia yangeweza kuzuia maendeleo ya uwezo wa watoto wao katika kipindi kingine. Vivyo hivyo, uaminifu fulani mkubwa ndani ya makundi ya ukoo uliowawezesha kushamiri katika hatua moja, baadaye unaweza kuwa vizuizi kwa umoja ndani ya mipangilio mipana ya kijamii. Na baadhi ya majukumu ya kijinsia yaliyoipambanua hatua ya mwanzoni ya maendeleo ya binadamu hatimaye yanaweza kuzuia maendeleo ya wanawake na ya jamii katika kipindi kingine. Mawazo na nadharia za nyakati zilizopita lazima zitathminiwe upya, ‘Abdu’l-Bahá hueleza. Binadamu “lazima sasa ajazwe sifa na nguvu mpya, viwango vipya vya maadili, uwezo mpya.” Kwa sababu “vipawa na baraka za kipindi cha ujana, ingawa vilikuwa sahihi na vyenye kutosheleza enzi za ujana wa mwanadamu, sasa havina uwezo tena wa kukidhi mahitaji ya ukomavu wake.” Changamoto iliyopo kwa jumuiya za Kibahá’í kote ulimwenguni, hivyo, ni kuchunguza desturi zilizopo sasa katika jamii zao, kuzipima kulingana na Mafundisho, kuondoa tabia zozote zisizohitajika na kujifunza kuanzisha mitindo mipya ya maisha ya familia inayoendana na mahitaji ya zama mpya.

3. Bila shaka, haiwezekani katika hatua hii ya mapema kuelezea asili ya mipangilio ya familia ambayo lazima hatimaye itokee katika ukamilifu wa Kipindi hiki Kitakatifu. Na jamii mbalimbali katika sehemu tofauti tofauti za ulimwengu, wakati zikitambua umuhimu wa familia imara, zinakabiliana na msululu wa nguvu ambazo huidhoofisha familia kwa namna mbalimbali Hata hivyo, mchakato wa ujifunzaji ambao huchangia kwenye mjongeo kuelekea mtindo mpya wa maisha ndani na miongoni mwa familia utachapuzwa kadiri ulimwengu wa Kibahá’í unavyokua kiuwezo kutumia baadhi ya umaizi muhimu kutoka katika Mafundisho.

4. Miongoni mwa maswali yatakayozingatiwa ni haya yafuatayo: Ni zipi sifa za maisha ya familia ya Kibahá'í na jinsi gani zinatofautiana na namna maisha ya familia yanavyoeleweka katika jamii ya leo? Ni ipi asili ya kipekee ya ndoa ya Kibahá'í na jinsi gani inakuza maisha ya familia? Jinsi gani familia za Kibahá'í zinavyochangia kwenye mchakato wa mabadiliko katika ujirani na vijiji, na zaidi? Ni vikwazo na vizuizi gani vinavyoizikabili familia za Kibahá'í ambavyo huwazuia kufikia shabaha hii? Jinsi gani muundo wa utekelezaji wa hatua ya sasa ya Mpango Mtakatifu unavyoimarisha maisha ya familia na kutengeneza fursa kwa familia zinazostawi kuchangia kwenye mchakato wa ujenzi wa jumuiya?

*

5. Dhana mpya ya familia huanza na dhana mpya ya ndoa. Bahá'u'lláh husema kwamba ndoa si tu "funguo ya kudumisha maisha kwa watu wa dunia", bali pia "ni chombo kisichoweza kuchunguzika cha utimizaji wa hatima yao."

6. Kwa Wabahá'í, ndoa si tu kifungo cha kimwili, bali pia ni cha kiroho, kikiwa na maana kwa maisha katika ulimwengu huu na ule ujao. Ndoa ya Kibahá'í, 'Abdu'l-Bahá hueleza, "ni ahadi ya pande mbili mmoja kwa mwingine, na muungano wao wa akili na moyo", ili waweze "daima kuboresha maisha ya kiroho ya kila mmoja," na ili waweze "kuishi pamoja kwa urafiki wa karibu kabisa" na "kuwa kama vile roho moja." Katika ndoa ya Kibahá'í, roho mbili hujifunza jinsi ya kusaidiana ili zote mbili ziweze kufikia kusudi lao la maadili yenye pande mbili—kukuza uwezo wao wa asili waliotunukiwa na Mungu na kuchangia kwenye ustaarabu unaoendelea daima. Uhusiano ambao wana-ndoa huuanzisha kuanzia sherehe yao ya ndoa, katika nafasi na wakati wote, utaathiri uundaji wa mahusiano mapya yasiyohesabika miongoni mwa watu wengine ambayo, kwa namna nzuri, yanaweza kubadilisha maisha na jamii.

7. Mtazamo wa Kibahá'í juu ya ndoa hupita mikinzano inayotokana na mitazamo ya uhuru na ya ukatazaji kupita kiasi inayoshuhudiwa katika jamii. Katika ndoa ya Kibahá'í, upendo, usawa, wenzi, uaminifu, uhusiano wa kimapenzi, uzazi na malezi ya watoto vimeunganishwa na uhusiano wao umeimarishwa yakianzisha ngome kwa ustawi binafsi na wa jamii. Mazoea huria ya kijamii hudhoofisha ndoa na familia kwa kuvitenganisha vipengele hivi ambavyo ni muhimu kwa ustawi wa mwanadamu, ambapo mazoea ya kurudi nyuma husisitiza kupita kiasi au kuharibu kipengele kimoja au vingine vya hivi ili kuwakandamiza wana-familia. Kufuata Mafundisho husaidia kutatua matatizo kama haya. Kuna mengi ya kujifunza katika mazingira anuwai ya kiutamaduni kote ulimwenguni kuhusiana na maana za sura zote za ndoa ya Kibahá'í zilizopatikana katika Mafundisho. Kwa mfano, jambo muhimu kwa maendeleo ya mtindo mpya wa maisha ya ndoa ya Kibahá'í ni kanuni ya usawa wa wanawake na wanaume. Kadiri kanuni hii inavyotumika kati ya mke na mume ndani ya ndoa, uhusiano unaimarika na kustawi, na wasichana na wavulana watalelewa kwa uelewa mpya wa usawa na utekelezaji wake wa kivitendo. Athari za kanuni hii hivyo zitaenda pole pole hadi kwa vizazi vijavyo na kuchangia kwenye maendeleo ya wanawake hadi matarajio ya 'Abdu'l-Bahá kwamba wanawake wata "shiriki kikamilifu na kwa usawa katika masuala ya dunia" yatimizwe kikamilifu.

8. Ndoa huunda familia. Na uhusiano mzuri utakaowaunganisha wana-familia wa familia ya Kibahá'í hutegemea juu ya haki na usawa. Kila mwana-familia lazima apate haki zake; kila mmoja lazima atimize majukumu yanayomhusu. "Kulingana na mafundisho ya Bahá'u'lláh, familia, ikiwa ni sehemu ya jamii ya binadamu, lazima ielimishwe kulingana na kanuni za utakatifu," 'Abdu'l-Bahá hueleza. "Uadilifu wa kifungo cha

familia daima lazima uzingatiwe, na haki za mwana-familia mmoja mmoja hazipaswi kukiukwa.” Uhusiano huu mzuri miongoni mwa wana-familia unahitaji kukuza kwa makusudi.

9. Katika familia ya Kibahá’í, wana-ndoa ni washirika wa kweli; hakuna mmoja aliyewekwa kuwa msaidizi wa mwingine. Kwa pamoja wanakumbana na changamoto za maisha—ziwe za kiroho, kimwili au kijamii—kupitia sala, kujifunza, ushauriano na tafakari juu ya vitendo. Fikiria, kwa mfano, maamuzi yanayohusiana na elimu ya watoto. Maandiko ya Kibahá’í yanamtambua mama kama mwalimu wa kwanza wa mtoto na kudumisha haki zake kuhusiana na hili. Kama asemavyo ‘Abdu’l-Bahá, “Kwa kweli ni kina mama ambao huamua furaha, ukuu wa siku zijazo, njia za adabu na elimu na maamuzi, uelewa na imani ya watoto wao.” Bado, baba pia anawajibika kwa ajili ya elimu na malezi yao, na hawezi kumuachia jukumu hili muhimu mama peke yake. Na wakati, kumsaidia mama katika jukumu hili na kuhakikisha hanyimwi haki kwalo, baba ana jukumu la ziada la kuisaidia familia kifedha, hii haimaanishi kwamba majukumu haya yamewekwa bila kunyumbulka. Kutokana na uelewa wao wa Mafundisho, wana-ndoa hutafuta njia bora zaidi ya kusimamia masuala ya kifamilia kulingana na hali za mtu binafsi na za kijamii. Kila hatua ya maisha ya ndoa itatoa changamoto na fursa zinazolingana ambazo wana-ndoa lazima wajitahidi kuzisimamia, kwa ushirikiano na kwa ufanisi, huku wakihakikisha maendeleo ya kiroho, kiakili na kitaalamu ya wote wawili; mke na mume.

10. Katika mazingira yenye msaada ya familia, wazazi hutoa miongozo makini kwa watoto wao ili wajifunze kuishi maisha yenye maana na yenye lengo la ibada, njema na huduma. Kwa kusudi hili, kupitia mfano wao na mtindo wa maisha na mwingiliano wao wa kila siku, hali kadhalika mazungumzo yasiyohesabika, wazazi kwa upendo hulea ndani ya watoto wao sifa, mitazamo, mienendo na uwezo uongezekao utata, wakitumia mbinu na njia zao katika kila hatua ya ukuaji wa mtoto, kuanzia ukembe hadi utu uzima. Kuanzia umri mdogo, watoto hujifunza kumgeukia Mungu na kumpenda Yeye, kusali na kutongoa Neno la Mungu kila siku, wakijiona kama roho bora kabisa zinazojitahidi kukuza sifa za kiroho, kupendelea wengine kabla yao wenyewe, na kuonesha sifa hizi katika uhusiano wenye kujali na ushirikiano. Kadiri waendeleavyo, wanajifunza kuzoea shida, kujifunza nidhamu binafsi na uwajibikaji, kuwa wasiojali nafsi, na kupata maarifa ya sanaa na sayansi. Na kadiri wanavyochangamana na dunia kwa namna yao, wanajifunza kukuza mwelekeo wa huduma, kueneza na kutumia mafundisho ya matakatifu, kuondoa tofauti na kushiriki katika ushauriano, kubakia imara katika Agano, kufanya kazi kwa ajili ya uboreshaji wa ulimwengu na kujielekeza wenyewe kwa yale mambo ambayo huleta heshima ya milele. Maandiko ya Kibahá’í huwapa wazazi chanzo kisichokuwa na kikomo cha umaizi wa kukuza mitazamo hii na mingine mingi muhimu, ujuzi na uwezo, na taasisi ya mafunzo hutoa msaada muhimu kwa familia kwa kuongeza uelewa na uwezo wa wana-familia wake wote. Pia kunaweza kutatikana rasilimali zingine za kusaidia katika elimu ya kijamii, kiroho na kimwili kwa vijana ambazo familia inaweza kuzitumia—shule, maisha ya kijamii, miradi ya huduma na kadhalika. Hata hivyo, jukumu kuu la kuhakikisha elimu sahihi na kamili ya watoto linabaki kwa wazazi.

11. Kadiri muda unavyopita, uhusiano miongoni mwa wana-familia hubadilika na kuchukua sura mbalimbali. Vifungo vinavyolelewa kwa uangalifu vya upendo na umoja miongoni mwa wana-ndugu hutoa msaada uinuao na wa kudumu, na huwa kama ngome dhidi ya wivu mdogo mdogo na migawanyiko ambayo yaweza kutokea katika maisha ya familia. Kwa udhahiri, haki na majukumu ya watoto wakubwa siyo

sawa kama yale walipokuwa wadogo. Wazazi wanapaswa wawe waangalifu kwa mabadiliko haya wanapowaandaa watoto wao kwa yale ya utu uzima, kwa makini wakikuza uhuru na uwajibikaji katika kizazi kijacho kadiri wakuavyo. Vijana huendelea, katika maisha yao yote, kuwaheshimu na kuwathamini wazazi wao, walakini kadiri wanavyokua, lazima wabebe jukumu la maisha na machaguo yao. wenyewe Kadiri muda unavyopita, majukumu haya hubadilika, na mazingira yanaweza kuendelea kumdai mtoto kutoa msaada kadiri wazazi wanavyozeeka.

12. Uhusiano wa familia kiini umejengwa katika mizunguko ya uhusiano unaoendelea kupanuka, ukianzia na familia pana. Mababu/bibi, ndugu wa kike na wa kiume wa upande wa baba na mama na binamu hutoa huduma na msaada unaosaidia kutimiza madhumuni na majukumu ya familia. Sifa za uhusiano wa familia kama hizi pia huenea hadi kwa Wabahá'í wenzake na marafiki wengine ambao wanaweza kuisaidia familia kwa njia mbalimbali. Katika mtandao wa karibu wa kijamii ulioundwa katika jumuiya changamfu, wazee hutoa ushauri wenye busara na wa kina, na mfano wa kipekee. Wengine hujiingiza kama shangazi na wajomba wa kiroho kushiriki huba na wasiwasi kwa ajili ya maendeleo ya vijana na kutoa msaada ambao huongeza juhudi na matarajio ya hali ya juu ya wazazi. Vijana huwa kama kaka na dada wakubwa ambao, kwa njia mbalimbali, huwasaidia na kuwapa hamasa wale walio wadogo kuliko wao wenyewe. Kwa namna hii, hisia ya umoja, ya upendo, kujali, imani na mshikamano ambayo awali hulelewa katika familia huanza kufunwa katika muundo wa uhusiano katika jumuiya.

13. Kujali mambo ya kifedha ni kipengele muhimu cha maisha ya familia yenye umoja na ustawi na yenye ushiriki wa familia katika jumuiya inayokua. Ushauriano kati ya mke na mume, na pamoja na watoto pale inapohitajika, utamua jinsi suala hili la kifedha litakavyolinganishwa na mambo mengine mengi na majukumu ya maisha ya familia. Usimamizi wa busara na makini wa fedha za familia lazima uzingatie mambo mengi, ikiwa ni pamoja na jinsi fedha zinavyopatikana, kutumika na kuwekwa akiba; jinsi elimu na ustawi wa watoto unavyoendelezwa; kiasi gani kinapaswa kitengwe kwa ajili ya Mfuko wa Imani au kusaidia masuala ya kijamii; na jinsi ya kutekeleza wajibu wa Ḥuqúqu'lláh. Katika kujibu maswali haya na mengine kama hayo, familia hutoa nafasi ya kujifunza kwa vitendo kuhusu ukarimu, uwajibikaji, tofauti kati ya mahitaji na matamanio, na usimamizi wa mali.

14. Maisha ya familia ya Kibahá'í hutoa jukwaa la mwingiliano mzuri na jamii pana zaidi. Mwingiliano huu hushamiri kadiri wana-familia wanavyojitahidi kuonesha katika maisha yao mafundisho ya msingi ya Kibahá'í. Kwa mfano, matumizi ya kanuni ya usawa wa wanawake na wanaume, ambayo tayari imekwishatajwa, hujenga uhusiano wa kipekee kati ya mke na mume hali kadhalika miongoni mwa watoto na familia kwa ujumla, na kuwaandaa wana-familia kuchangia kwenye kuchangamana katika jamii ambayo huachilia uwezo wa wote. Vivyo hivyo, kufuata kanuni ya umoja wa binadamu kunahitaji watoto wapatiwe tajiriba inayowalinda dhidi ya ubaguzi wa aina zote na kukuza utambuzi wao wa utofauti, jambo linalochangia uwezo wa kujenga uhusiano wa umoja na mshikamano katika ulimwengu uliogawanyika. Kwa nyongeza, kukuza uwezo kwa ajili ya kuchunguza ukweli, kwa ajili ya kutambua upatano wa sayansi na dini, kwa ajili ya kutatua tofauti za maoni na kufanya maamuzi kupitia ushauriano na ushirikiano badala ya mivutano na mashindano huwawezesha wana-familia kama wahusika wenye ufanisi katika mchakato wa mabadiliko ya kijamii. Na kukuza sifa kama vile haki na huruma miongoni mwa wana-familia kunawaandaa watoto kuanzisha uhusiano thabiti na mlinganifu pamoja na wengine katika jamii. Hivyo, juhudi ya kujifunza kutumia Mafundisho ndani ya familia hufanya

yote mawili; huzalisha ndani ya watoto maono ambayo huipita sana familia yenyewe na kuinua uelewa kuhusu hali na mahitaji ya jamii ya watu wa dunia.

15. Kukuza mtindo mpya wa maisha ya familia pia hukumbana na nguvu za uchangukaji ambazo ni sura isiyoweza kutenganishwa na zama zilizo katika kipindi cha mpito. Nguvu hizi zinazoishambulia jamii hususan zimeziathiri familia, zikivunja vifundo vyake na kuleta athari kubwa kwa wanajamii wake, hasa watoto. Zinaweza kuwasababishia wana-familia baadhi ya magonjwa ya kijamii yenye uharibifu mkubwa: kutokuwepo kwa upendo na kujali, kutokujali mambo ya roho, kutokuwa na utu, umasikini, ukosefu wa usalama na vurugu. Watu hushawishika kukubali maisha ya utapanyaji mali au kujifurahisha nafsi, hivyo kuwa vitu tu vya kuchezewa na wale wanaotafuta kushinikiza mipango yao kwa jamii. Itikadi na utambulisho vinavyopingana, visivyoendani na mawazo bora ya umoja wa binadamu na ulimwengu wenye amani, hushindania uaminifu wa umma na kushindana baina yao kwa ajili ya ukuu. Baadhi ya harakati hizi hupandikiza mbegu za ubaguzi na misimamo mikali ambazo mwishowe husababisha utengano, uhasama na mashindano miongoni mwa jamii ya watu wa ulimwengu. Zingine zinaweza kuonekana kuendana na baadhi ya vipengele vya Mafundisho, zikiwaondoa tu marafiki mbali na njia iliyonyoka ya Bahá'u'lláh. Nguvu zinazohusiana na mchakato wa uchangukaji huathiri makundi tofauti ya watu kwa namna tofauti. Familia na jumuiya kwa ujumla, itahitaji kujifunza kutathmini hali zilizopo, kuelewa asili na athari za nguvu hizi, na kwa kutegemea kabisa msaada mtakatifu, kukuza hatua za kukinga na kurekebisha ili kuhimili dhoruba zenye ghasia za zama hizi za hatari.

16. Uhusiano wa karibu zaidi wa wana-familia na shauku yao ya dhati kuwahudumia wengine hufungua nafasi ya kipekee ya kijamii: nyumba ya Mbahá'í. Nyumba changamfu ya Kibahá'í ni jambo lisiloweza kisichofidika katika mchakato wa ujenzi wa jumuiya mashinani. Katika mazingira ya upendo ya nyumbani, wana-familia husaidiana kuwa wahusika wakuu wenye uwezo na kujiamini wa Mpango Mtakatifu, na wanawakaribisha na kuwasaidia wengine kuchukua jukumu la kuibadilisha jamii. Katika nyumba ya Kibahá'í, ukarimu mkunjufu huchanganywa na uhuishaji wa kiroho na maendeleo ya kiakili. Kupitia shughuli ambazo kila familia ya Kibahá'í inaweza kufanya nyumbani kwake, inaweza kuonesha namna ya maisha ambayo yanaweza kuigwa na wale wote wanaotaka kupambana na nguvu gawanyishi ambazo huchochea kutoridhika, migogoro na maslahi binafsi, na kufuma vifungo vya imani, ushirikiano na hatua chanya ambazo kwazo jumuiya yenye siha njema huitegemea. Kwa hakika, katika klasta mbalimbali kote ulimwenguni, makundi ya familia tayari yanafungua nyumba zao na kufanya kazi kwa pamoja ili kusaidia kuimarisha shughuli za maeneo yao na kupanua mawanda na ushawishi wao kwa kiwango kikubwa.

17. Dhana ya maisha yenye kufungamana ya huduma ni muhimu kwa maisha ya familia kama ilivyo kwa maisha ya mtu binafsi. Mahitaji na fursa tata ambavyo familia hukabiliana navyo huendelea kubadilika kila wakati. Kwa ujumla, kuendelea pamoja kwenye njia ya huduma kunaiimarisha familia, na kuisaidia kukabiliana na majukumu yake mengi katika kila hatua ya maisha ya wana-familia wake. Nyakati zingine, inapojitokeza fursa ya huduma yenye uhitaji zaidi—iwe kwa mwana-familia au kwa familia nzima—vifungo vya msaada ndani ya familia ya Kibahá'í iliyojitoa vinaweza kuikumbatia kwa moyo mkunjufu kadiri iwezekanavyo juhudi kama hiyo ya kujitoa. Nyakati kama hizo ni muhimu kukumbuka asili ya dhabihu, ambayo, kama anavyoeleza 'Abdu'l-Bahá, ni kuachana na wasiwasi wa hali ya binadamu kwa ajili ya mambo ya Mungu. Dhabihu hufanya huduma kubwa zaidi iwezekane, lakini sio familia yenyewe inayopaswa kutolewa dhabihu.

*

18. Wakati tunapochunguza maendeleo ya Mpango wa Miaka Tisa, tunajawa na kicho na shukrani za kina kwa kazi za kujitoa za marafiki. Katika mazingira anuwai kote ulimwenguni, tunashuhudia juhudi nyingi za kujitoa zinazotokana na ushirikiano wa watu binafsi, jumuiya na asasi, huku marafiki wakiwahusisha watu wenye shauku katika mchakato wa kujenga jumuiya, wakianzisha mlolongo wa miradi kwa ajili ya elimu na uboreshaji wa jamii, wakipeleka kazi ya Imani hadi kwenye maeneo mapya, na kuunganisha ahadi nyingi zilizomo katika maisha ya huduma yenye umoja. Na licha ya vizuizi vya ukandamizaji au mabadiliko ya ulimwengu uliovurugika, marafiki husisitiza shabaha zao bora kabisa. Roho zisizo na idadi kote ulimwenguni zinapambana, ndani ya mipaka ya mazingira na uwezo wao, kuachilia nguvu ya Imani ya ujengaji jumuiya kwa viwango vikubwa zaidi. Kwa malengo haya, wajibu unaotimizwa na familia za Kibahá'í utaendelea kuwa muhimu na wenye athari kubwa zaidi katika miaka na miongo ijayo. Marafiki wote wana mchango muhimu wa kutoa ili kuimarisha kipengele hiki cha msingi cha maisha ya Kibahá'í.

19. "Nyumba yangu ni nyumba ya amani", inaripotiwa kusemwa na 'Abdu'l-Bahá. "Nyumba yangu ni nyumba ya furaha na shangwe. Nyumba yangu ni nyumba ya vicheko na nderemo. Yeyote aingiaye kupitia malango ya nyumba hii, lazima aondoke na moyo wenye furaha. Hii ni nyumba yenye nuru; yeyote aingiaye humu lazima awe ameangaziwa." Acheni familia na nyumba zenu, marafiki wapendwa, ziendelee kuwa kimbilio na nguzo ya kuwahimili wanadamu wote.

Imesainiwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu